

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA

16 MEI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA – TAREHE 16 MEI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI MKUU:

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Nchini ya Mwaka 2023.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**352. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY
KISWAGA (MAGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara za Mitaa kwa kiwango cha lami katika Mji wa Kisesa - Bujora - Magu.

353. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini ahadi ya ujenzi wa Barabara ya Kilometa 3 kwa kiwango cha lami katika Mji wa Kikonko itatekelezwa.

354. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kutengeneza Barabara ambazo zimeharibika Wilayani Chunya.

355. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza tena kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kupitia Halmashauri.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

356. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (BLW):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kwa vipi Mabadiliko ya Tabianchi yanasababisha uvamizi wa wadudu waharibifu kwa mazao mbalimbali.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

357. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, kwa kiwango gani Serikali inahakikisha Bodaboda wanapata Mikataba ya pikipiki isiyo ya kinyonyaji kutoka kwa wakopeshaji binafsi.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

358. MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itapeleka huduma za utoaji wa Vitambulisho vya Taifa katika Halmashauri ya Busokelo.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

359. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Mkandarasi aliyeteuliwa kujenga Soko la Samaki Manda - Ludewa ataanza kazi.

WIZARA YA FEDHA:

360. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL MWENISONGOLE (MBOZI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, kwa nini TRA inalazimisha Vyama vya Msingi vya Ushirika kutumia EFD mashine wakati hawafanyi biashara na mauzo yao ni mara moja kwa mwaka.

WIZARA YA KILIMO:

361. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI BUSHIRI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha Zao la Pamba Mkoani Kilimanjaro.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

DODOMA
16 MEI, 2024

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE